

# **BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA**



## **TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA CCC) litaiza kwa njia ya mnada wa hadhara mali chakavu **siku ya Jumamosi, tarehe 14 Januari, 2023** kuanzia **saa tatu asubuhi** katika Ofisi za Baraza zinazopatikana Kinondoni karibu kabisa na Ubalozi wa Ufaransa. Mali hizi chakavu zinajumuisha vifaa vya tehma , vifaa vya Ofisi na samani za Ofisi.

### **MASHARTI YA MNADA**

- Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo.
- Atakayetaja bei ya juu kabla ya nyundo kugongwa ndiye atakayeuziwa kifaa.
- Aliyetaja bei ya juu siyo lazima auziwe kama bei hiyo haijafikia bei elekezi.
- Kwa vifaa na samani,Mnunuzi atatakiwa kulipa papohapo asilimia mia moja (100%) ya thamani ya chombo/kifaa alichonunua.Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo/kifaa husika.
- Mnunuzi ataruhusiwa kuchukua vifaa vyake kutoka eneo la Baraza lililotajwa hapo juu baada ya kukamilisha malipo yote.

**LIMETOLEWA NA:  
KATIBU MTENDAJI,**

**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA ,**

**JENGO LA WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA),**

**MAKUTANO YA BARABARA YA ALI HASSAN MWINYI NA KILIMANI,**

**S.L.P 12242,**

**DAR ES SALAAM.**

***Kwa Maelezo zaidi piga simu 0742 427747***